



ZAO LA ILIKI (CARDAMOM)



Utangulizi

Iliki ni moja kati ya mazao ambayo yanatumika sana karibia kila siku kwenye matumizi ya nyumbani, hutumika kama viungo kwenye chai, chakula na pia kama tiba ya magonjwa mbalimbali

Mazingira yanayofaa kwa kilimo cha iliki

Hali ya joto

- Kiasi cha nyuzijoto 10-25
- Hata hivyo kukiwepo kivuli cha kutosha iliki inakuwa pia katika nyuzijoto 30.

Mwinuko kutoka usawa wa bahari

- Kuanzia mita 650 hadi mita 1500

Mvua

- Iliki husitawi vizuri katika maeneo ambayo hupata mvua kati ya milimita 1,500 hadi 3,000 kwa mwaka.

Udongo

- Iliki hupenda udongo wenye rutuba nyingi na hasa mboji au maozea ya mimea ya misituni

Kivuli

- Iliki haipendi jua la moja kwa moja kwa hiyo miti ya kivuli ni muhimu kuwepo shambani.

Miche

- Iliki inaweza ikapandwa kwa kutumia mbegu, lakini huchelewa sana kuzaa.
- Machipukizi ndiyo hutumika sana kama miche Ingawa njia hiihuchangia sana kusambaza wadudu na magonjwa
- Machipukizi yakipandwa huaanza kuzaa baada ya miezi 18.
- Machipukizi ya kupanda yanahitaji kuwa na macho 4.



Kitalu cha miche ya iliki

Kupanda

- Ni vizuri kupanda wakati wa mwanzo wa mvua za masika

Nafasi ya upandaji

- Ikipandwe katika nafasi ya mita 2 hadi 2.5 kati ya mimea na mita 2.5-3 kati ya mistari.

Umbile

- Iliki ni mmea wenye mizizi mifupi na shina lake hutoa machipukizi mengi ambayo ni laini. Kwa sababu mizizi ni mifupi, ni rahisi sana kuharibika kwa jua wakati wa ukame na


kusababisha kufa miche mingi endapo hakuna kivuli cha kutosha.

Aina za iliki.

Kuna aina kuu mbili za iliki ambazo ni

1. Malabar

- Aina hii huzaa kwa kutambaa ardhini na matunda yake ni madogo madogourefu wa mmea wa malabar ni karibia mita 3.
- Hustawi zaidi ukanda wa mita 650 hadi mita 950 kutoka usawa wa bahari.



Iliki aina ya Malabar

2. Mysore

- Aina hii matunda yake huzaliwa kwa wima, ina majani mapana na mmea una urefu zaidi ya mita3.
- Hustawi zaidi ukanda wa juu wa mita 950 hadi 1,500 na podo zake ni ndefu, masuke yake husimama.



Iliki aina ya Mysore

Kupanda

- Tengeneza mashimo ya sm 60 x 60 na panda miche kwenye mashimo.

Matunzo

- Palilia mara kwa mara, weka matandazo kuzuia magugu yasiote,
- Ni muhimu kurekebisha miti ya kivuli kwa kupunguza matawi na kupanda miti katika eneo ambalo liko wazi sana.



Shamba la iliki lilitotunzwa vizuri

Wadudu waharibifu

Thrips (vithiripi)



Wadudu hawa hufyonza maji katika matunda machanga hatimaye mmea hudhoofu na kufa kwa urahisi.

Tiba,

- Zuia kwa kusafisha shamba na kama mashambulizi ni makubwa basi tumia dawa za asili.

Magonjwa

- Iliki huwa na ugonjwa wa kuoza majani na matunda machanga na unasababishwa na jamii ya ukungu.

Tiba

- Zuia kwa kuliweka shamba katika hali ya usafi,
- Dhibiti kwa kupiga dawa

Virus (mosaic virus)

- TibaDhibiti kwa kutumia aina inayo vumilia na pia mbegu bora ili kuepuka usambazaji

Wanyama waharibifu

Wanyama kama kenda,nyani,panya na kima huwa wanakula iliki na kuziharibu

Tiba

- Zuia kwa kuliweka shamba katika hali ya usafi na kulinda wanyama wasiharibu.

Kuvuna

- Iliki huchukua mwaka mmoja na nusu hadi mitatu tangu kupandwa mpaka kuvuna pale unapopanda miche midogo.
- ukipanda mbegu huchukua miaka minne hadi mitanompaka kuvuna
- Iliki huvunwa kwakuchuma matunda yaliyokomaa na kuyaacha ambayo bado yakiendelea kukomaa.
- Matunda yaliyopevuka huwa na rangi ya manjano iliyochanganyika na kijani pia huonekana yamevimba.



Iliki iyovunwa

Kupanga madaraja

Kuna daraja kuu mbili na inatokana na utaratibu wa ukaushaji narangi ya mwisho baada ya kukauka.

- Endapo itakaushwa kwa kutumia jua iliki itakuwa na rangi ya kijivu iliyochanganyika na nyeupe na daraja lake litakuwa la pili.

- Ikikaushwa katika matanuri basi rangi ya mwisho itakuwa ya kijani na daraja lake litakuwa la kwanza na hili ndilo daraja lenye bei kubwa.

Kwango cha mavuno

- Shina moja hutoa hadi kilo moja kwa mvuno mmoja na kwa mwaka huvunwa mara 2 kwa mazingira mazuri.
- Kwa hiyo shina moja linaweza kutoa kilo 2 kwa mwaka. Katika ekari moja kwa nafasi ya mita 2x3 yapo mashina 667 ambayo yanaweza kutoa kilo 1,333 kwa mwaka.

Matumizi

- Kiungo kwenye chakula
- mchanganyiko kwenye madawa, mafuta na vipodozi
- kutengeneza vinywaji

Soko la Iliki

- Iliki ina soko kubwa wakati wote, kwani huzalishwa katika baadhi ya maeneo, huku mahitajii yake yakiwa ni makubwa kulingana na idadi ya watu, na matumizi yake.

Faida ya Iliki kiafya

- husaidia kuipa uwezo mzuri figo wa kuondoa taka ndani ya mwili, huku ikisaidia kuweka sawa mfumo wa umeng'enyaji chakula tumboni.
- Kuondoa kiungulia, gesi tumboni pamoja na kusaidia wenye shida ya kukosa choo kwa muda mrefu.

- **Imeandaliwa na**

- **Kitengo cha Utafiti wa Viungo TARI-**

Mlingano,

- **S.L.P 5088, TANGA.**

- **Simu: +255 688 150 745**

- **Barua pepe: cdmlingano@tari.go.tz**

-